

# MAIR

Ripoti ya Mwaka ya Utekelezaji  
MKUKUTA - 2006/2007



**Nguzo ya Tatu:**  
**Utawala Bora na Uwajibikaji**

Nguzo ya tatu ya MKUKUTA inahusu shughuli zinazo lenga kukuza, “Utawala Bora na Uwajibikaji”. Matokeo ya jumla ni (a) Utawala bora na Utawala wa Sheria (b) Uwajibikaji wa Viongozi na watumishi wa umma, (c) Demokrasia na uvumilivu wa kisiasa na kijamii, na (d) Amani, Utulivu wa kisiasa, umoja wa kitaifa na mshikamano wa kijamii.

## **Malengo**

- Kuhakikisha kuwa miundo na mifumo ya utawala pamoja na utawala wa sheria ni vya kidemokrasia, shirikishi, uwakilishi, uwajibikaji na ujumuishaji.
- kuhakikisha ugawaji sawa wa rasilimali za umma pamoja na kushughulikia rushwa ipasavyo.
- kuweka mfumo wa huduma za umma unaofaa kama msingi wa kuboresha utoaji wa huduma na kupunguza umaskini.
- kuhakikisha kwamba haki za maskini na vikundi vilivyo katika mazingira hatarishi zinalindwa na kukuzwa katika mfumo wa haki.
- Kuongeza ushiriki kijamii na kisiasa na Kupunguza kutovumiliana kisiasa na kijamii.
- kuboresha usalama binafsi na wa mali, kupunguza uhalifu na kuondoa unyanyasaji wa kijinsia na unyanyasaji majumbani.
- kuendeleza na kuimarisha utamaduni wa watu kama utambulisho wa kitaifa.

## **Changamoto kuu**

- Upungufu katika mfumo wa Kisheria.
- Kutekeleza kikamilifu maboresho ya sekta ya sheria.
- Usimamizi wa upelekaji wa madaraka, majukumu na rasilimali kwa wananchi.
- Kuboresha haki za binadamu.
- Kuongeza matumizi bora zaidi ya mbao za matangazo.
- Matumizi sahihi na bora zaidi ya teknolojia ya habari na mawasiliano.

## **Mambo tuliyojifunza**

Maboresho kwenye nguzo hii yanaweza kusaidia kufikiwa kwa malengo ya nguzo nyingine (ya kwanza na ya pili). Tumejifunza mambo makuu matatu:

### ***Matumizi Duni ya Taarifa za Umma:***

Ofisi za serikali zinatoa taarifa kwa ajili ya umma, lakini kumekuwepo na hamasa ndogo miongoni mwa wananchi katika ngazi ya jamii kutumia taarifa hizo. Kuna umuhimu wa kuzirahisisha taarifa hizo. Mambo ambayo jamii inapenda kupatiwa taarifa ni mengi ikiwa ni pamoja na:

- Watu wenye vyeti vya kimila vya umiliki wa ardhi katika ngazi ya kaya kwa kuzingatia jinsia.
- Mazingira ya kazi ya watumishi wa vyombo vya dola.

### ***Vita dhidi ya Rushwa***

Serikali itaendeleza juhudi zake za Kupunguza rushwa. Juhudi hizo ni pamoja na:

- Uhamasishaji wa kubadili mitazamo ya watumishi wa umma
- Kuimarisha ukaguzi wa taasisi za umma ili kupunguza matumizi mabaya ya raslimali
- Kuimarisha uwezo na utayari wa wananchi kuwa makini na kufuatilia michakato ya uwajibikaji wa ofisi za umma.

### ***Uoanishaji***

Masuala yanayohitaji kuoanishwa ni pamoja na:

- Mchakato wa kupeleka madaraka, majukumu na raslimali kwa wananchi ili kuhakikisha uthabiti, uendelevu na utekelezaji wenye ufanisi.
- Uratibu rasmi wa maboresho mbalimbali (Sekta ya Sheria, Sekta ya Utumishi wa Umma na Programu za Maboresho ya Serikali za Mitaa n.k.).
- Migongano katika baadhi ya sheria za kisekta.

## Hatua za kuchukua

Hatua zinazopaswa kuchukuliwa zinahusisha kukabiliana na changamoto zilizotajwa hapo juu. Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine watapaswa:

- Kuongeza uhamasishaji katika jamii kuhusiana na umuhimu wa taarifa.
- Kutoa mafunzo zaidi juu ya maadili na uaminifu kwa wataalamu ili kuimarisha utawala bora na uwajibikaji.
- Fanya utafiti wa viashiria vikuu ili kusaidia ufuatiliaji na tathmini ya baadaye.
- Boresha mazingira na miundombinu ya kazi.
- Shirikisha wadau wasiokuwa wa kiserikali katika kuimarisha uwajibikaji ikiwamo kupitia matumizi ya mbao za matangazo
- Ajiri wafanyakazi wapya na kuwapatia mafunzo kazini kila inapohitajika.
- Punguza mrundikano wa kesi mahakamani.
- Boresha miundombinu ya mawasiliano.
- Weka mfumo bora wa utawala bora, uwajibikaji na uwakilishi.
- Washirikishe zaidi wananchi katika kusimamia maliasili.
- Jenga uwezo wa watumishi wa Serikali za Mitaa katika kusimamia rasilimali na kutoa huduma bora.
- Panua na kuboresha magereza na kuweka mfumo wa taarifa za wahalifu.
- Weka mfumo mzuri na madhubuti wa kudhibiti na kufuatilia mipaka ya nchi.
- Imarisha Programu ya Huduma za Jamii na ya Zima moto na Uokoaji katika mikoa yote.

**Kwa maelezo zaidi wasiliana na:**

Wizara ya Fedha na Uchumi,  
S..L.P. 9111, Dar Es Salaam

Simu: +255 2111174, Fax: 21103226

Barua Pepe: [mkukuta@gmail.com](mailto:mkukuta@gmail.com); Tovuti: [www.povertymonitoring.go.tz](http://www.povertymonitoring.go.tz)